TANGAZO LA SERIKALI NA. 28 la tarehe 17/02/2017.

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1) (b))*

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA (MAREKEBISHO) ZA MWAKA, 2017

Jina na tarehe ya Kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa mfuko wa afya ya jamii) (Marekebisho) za Halamshauri ya Wilaya ya Kyela za mwaka 2017, na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa mfuko wa afya ya jamii) za Halamshauri ya Wilaya ya Kyela za mwaka 2004 ambazo kwenye Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamalaka ya Halmashauri ya wilaya ya Kyela;

Marekebisho (Tangazo la Serikali Na. 388/2004)

3.Sheria Ndogo hizi zinarekebisha kifungu cha 22(1) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuyaondoa maneno yafuatayo;

"kila kaya itachangia kiasi cha shilingi (10,000/= kwa mwaka " na badala yake kuweka maneno "Kila mwanachama katika kaya atachangia kiasi cha shilingi elfu tano (5,000/=) kwa mwaka"

Muhuri wa Halmashauri ya kyela ulibandikwa kwenye Sheria hizi ndogo kufuatia Azimio la Halmashauri lililopitishwa katika mkutano wa baraza la madiwani ulioitishwa na kufanyika tarehe 31.07.2014 na ulibandikwa mbele ya:-

C.R. KASONGO,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*(W) Halmashauri ya Wilaya ya Kyela*

GABRIEL M.KIPIJA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*